

# Msingi wa Mungu Usiotikisika

Tunapofikiria hali ya dunia tunayoishi ndani yake, mahali vita na migogoro vinaonekana kutawala kila kituo cha habari, majanga ya asili yanawakumba watu duniani na mahali ambapo mahusiano yaliyo vunjika ni ya kawaida ndani ya jamii, tunatazama Zaburi 46, inayotupa ujasiri kwamba Mungu ndiye msingi usiotikisika katika mazingira yoyote.

Zaburi 46 inatukumbusha Mungu ni nani na tumaini letu linapatikana wapi. Tunaweza kukumbuka wema wa Mungu na uaminifu wake kwetu. Bila kujali mazingira yetu, bado tuna sababu ya kusifu.

Tunabadilika, mazingira yetu yanabadilika, lakini Mungu wetu habadiliki.

# Zaburi 46

*Kwa kiongozi wa muziki wa wana wa Kora.*
*Sawa na alamoth. Wimbo.*

1 Mungu ndiye kimbilio na nguvu,
Msaada utakaoonekana tele wakati wa mateso.

2 Kwa hiyo hatutaogopa ijapobadilika nchi
Ijapotetemeka milima moyoni mwa bahari,

3 maji yake yajapovuma na kuumuka
Ijapopepesuka milima kwa kiburi chake.

4 Kuna mto, vijito vyake vyaufurahisha mji wa Mungu,
Patakatifu pa maskani zake Aliye Juu.

5 Mungu yu katikati yake hautatetemeshwa;
Mungu atausaidia asubuhi na mapema.

6 Mataifa yalighadhibika, falme zikataharuki;
Alitoa sauti yake, nchi ikayeyuka.

7 Bwana wa majeshi yu pamoja nasi;
Mungu wa Yakobo ni ngome yetu.

8 Njoni muyatazame matendo ya Bwana,
jinsi alivyofanya ukiwa katika nchi.

9 Avikomesha vita
hata mwisho wa dunia.
Avunja uta, akata mkuki;
achoma moto magari.

10 Acheni mjue kuwa mimi ni Mungu;
Nitakuzwa katika mataifa,
nitakuzwa katika nchi.'

11 Bwana wa majeshi yu pamoja nasi;
Mungu wa Yakobo ni ngome yetu.



Mungu asiyetikisika ndiye
Kimbilio Langu

Maandiko: Zaburi 46:1-11 Malaki 3:6

Zaburi 46.

Tamko la kuabudu kutoka kwa taifa la Israeli, Zaburi ya kusifu nguvu za Mungu na uwepo wake kwa watu wake wakati wote. Zaburi 46 inaonyesha muujiza wa ukombozi wa Mungu kwa watu wake na hali yake ya kutokubadilika katika mazingira ya kukatisha tamaa sana.

Maneno ya Zaburi hii ni ukumbusho mzuri kwamba Mungu hatuachi wakati mazingira yakiwa magumu. Yupo hapo hapo pamoja nasi, na habadiliki.

Mungu wetu ambaye yupo wakati wote yeye haathiriki na changamoto za dunia hii, nguvu zake na uwepo wake havitaweza kubadilishwa kwa kuhamisha maadili, mawazo tofauti au dunia isiyo imara.

Wakati mazingira ya maisha yanatishia kutulemea, tunaweza kupata kimbilio na pumziko katika Mungu wetu apatikanaye mda wote na asiyebadilika. Tunaweza kushikilia ufahamu kwamba Mungu yuko pamoja nasi na kwa usalama wa kutambua kwamba nguvu za Mungu hazitishwi na majanga asilia (Zaburi 46:2-3) wala vita (Zaburi 46:8-9).

Mungu amehakikisha uwezo wake wa kutuangalia na kututunza sisi, Tunapokuwa wazi kwake, yeye siyo mzito wa kuona au kutambua, yeye yuko karibu na anapatikana. Tunaweza kuamini kwamba yeye ni Mungu pamoja nasi naye atabakia yule yule. Katikati ya vurugu na maangamizo, yeye hutoa mahali salama, amani, na ulinzi.

Tunaweza kupata kimbilio katika Bwana mweza yote, kimbilio letu na nguvu, msaada unaopatikana tele wakati wa mateso.

*Baba wa Mbinguni,*

*Katikati ya kutokuwa na uhakika, tunapata hakikisho katika uwepo wako usiobadilika. Wewe ndiye kimbilio na nguvu zetu, msaada utakaopatikana tele wakati wa mateso. Twaomba tupate faraja katika uhakika wa uwepo wako na maarifa ya pendo lako lisiloshindwa.*

*Amina.*

Soma vifungu vya Zaburi 46 mara kadhaa. Vifungu hivi inaweza kuwa umevizoea. Visome taratibu na kwa makusudi.

Unapofikiria kuhusu maisha yako na dunia unamoishi, ina maana gani kwako kuthibitisha kwamba Mungu ni kimbilio, nguvu yako, yuko pamoja nawe naye atakusaidia unapokabiliana na matatizo?

Hii hukufanya ujisikie namna gani?

Unahitaji kukumbuka nini kutoka kwenye kutafakari kwako Zaburi 46 leo? Chukua muda kiasi kuandika au kurekodi mawazo yako.



Mungu Asiyetikisika Hunipa
mimi Ujasiri

## Maandiko: Zaburi 46:1-11

'Kwa hiyo, hatutaogopa, ingawa dunia inatoa nafasi na milima inaanguka ndani ya moyo wa bahari'.

Sisi hatutaogopa.

Haya madai ya ujasiri. Madai ambayo sio kila mara ni rahisi kuwa dhahiri katika maisha yetu, hasa tunapoona machafuko, kutokuwa na uhakika, hatari na mateso katika dunia yetu, katika familia zetu na katika jamii zetu.

Hofu ni mwitikio wa asili wa binadamu, na ni majibu yanayoweza kutusukuma kwenye matendo yasiyofikirika au kutuzuia sisi kutembea kabisa. Hofu ya usalama wetu, hofu ya matokeo, hofu ya yasiyojulikana. Hofu inaweza kulemaza.
Kuna wakati ambao mambo yanayotokea kutuzunguka, mazingira katika maisha yetu wenyewe au hadithi tunazoziona katika majarida huonekana kuwa hayawezekani kukabiliwa. Tunaweza tukajikuta tunauliza:

Mungu yuko wapi katika yote haya?

Kwanini Mungu hayazuii haya kutokea?

Nini kitatokea kwangu na kwa wale ninaowapenda?

Kuna nyakati hatutaelewa kile kinachoendelea kutuzunguka sisi. Tunaweza kuuliza maswali haya lakini tunaweza tusipate majibu.

Kuna nyakati kutoogopa, na kuwa jasiri vinaonekana kuwa sio rahisi. Lakini wema wa Mungu hautegemei tunavyojisikia.


Hizi ndizo nyakati ambazo lazima tuwaegemee wengine wanaotusaidia, wale wanaosimama kwa mshikamano na sisi. Tunaposikia sauti zinazoaminika, sauti za wale tunaowafahamu na kuwapenda, zikitangaza wema wa Mungu na uaminifu wake, tunaweza kupata tumaini na nguvu katika kuwaamini wao na upendo wao. Tukijizungushia mambo yanayotukumbusha Mungu ni nani na ahadi zake kwetu, tunaweza kupata ujasiri wa kuendelea kuamini.

Hatutakiwi kuwa na hofu. Kwanini? Kwasababu Mungu ndiye kimbilio letu, nguvu yetu, msaada wetu wakati wa mateso. Na yeye yuko pamoja nasi.

*Mpendwa Bwana,*
*Wakati kila kitu kunizunguka kinaponichanganya na kuniogopesha, asante kwamba wewe ndiye Mungu asiyetikisika anayenifahamu mimi na anayeelewa ninavyojisikia. Wewe ndiye anayenipa ujasiri nikabiliane na hofu zangu na anayenisaidia kunifanya niendelee, hata wakati maisha yanapoonekana kuwa magumu. Napumzika kwa kufahamu kwamba wewe upo pamoja nami.*

*Amina.*

Ni zipi hizo sauti za
kuaminika zinazotangaza
wema na ahadi za Mungu
katika maisha yako?



Je, wewe unaweza kuwa sauti
inayoaminika kwa mtu mwingine?
Anayehitaji wewe uwe sauti
inayoaminika kwake mda huu?



Naweza Kumwamini Mungu
Wangu Asiyetikisika

Maandiko: Zaburi 46:1-11 Zaburi 107 Zaburi 116
Kumbukumbu la Torati 26:5-11 Mathayo 28:20

Mwandishi wa Zaburi 46 anatuhimiza tukumbuke kile ambacho Mungu amefanya na, kama tunavyokumbuka, kujifunza kumwamini Mungu katika maisha yetu yajayo.

Watu wa Israeli waliacha nafasi katika maisha yao ili kukumbuka, akilini njia ambazo Mungu ameingilia kati katika historia kwa ajili ya mema yao (Kumbukumbu la Torati 26:5-11). Ilikuwa kipengele cha kati cha ibada yao na kilitoa utambulisho wao.

Kumwamini Mungu aliyetoa kwa ajili ya mahitaji ya watu, anayejitokeza na kutoa wokovu, kueneza Agano la Kale na kufikia utimillifu katika Agano Jipya kupitia kwa kazi ya kuokoa ya Yesu.

Unaweza kukumbuka kwamba Yesu, Mungu katika hali ya mwanadamu analeta uhakika. Yesu anafahamu kuwa na furaha maana yake nini na maumivu ya moyo, kulia na kucheka na huzuni. Anafahamu maana yake nini kuchoka, kuwa na njaa na kusherehekea.

Tunapokuja mbele zake Mungu, hatuhitaji kuja na kilichosafishwa, tolea la maneno sahihi yaliyo moyoni. Yesu anafahamu inafananaje kuwa mwanadamu. Tunakuja kwa ukweli kama tuwezavyo, tukifahamu kwamba anatusikia na kutuelewa.

*Mpendwa Bwana,*

*ninavyokumbuka uaminifu wako kwangu huko nyuma, napata uhakika wa msaada wako na wokovu. Asante kwamba hali yangu ya sasa sio kwamba haijulikani kwako. Wewe ndiye Mungu asiyetikisika, nami naweka tumaini langu kwako.*

*Amina.*

# ‘NJONI MYATAZAME MATENDO YA BWANA, JINSI ALIVYOFANYA UKIWA KATIKA NCHI.’

Chukua muda utafakari kuhusu maisha yako.

Unaweza kuchagua kuyagawa katika miongo au nyakati maalum. Kumbuka nyakati ambazo ulitambua uwepo wa Mungu.

Kumbuka yale ambayo Mungu amekutendea ndani na kwa ajili yako.

Unaweza kujifunza nini kutokana na haya kinachoweza kuleta uhakika kwa wakati uliopo na wakati ujao?

Wakati Uliopita

Sasa

Ujao



Ujasiri wangu uko katika
Mungu asiyetikisika

Maandiko: Zaburi 46:1-11 Luka 24:13-35

Zaburi 46 inaishia na ukumbusho kwamba tunapomzingatia Mungu, tutaona uwezo wake katika kila hali na katika kila hatua ya maisha yetu. Inatukumbusha kwamba Mungu ni Mungu, na Mungu yuko pamoja nasi. Tumehakikishiwa uwepo wa Mungu hata katika zile nyakati ambazo mazingira yetu binafsi au matukio ya dunia yanachukua sehemu kubwa ya maisha yetu na nguvu mpaka tunaona vigumu kutambua kwamba Mungu yupo pamoja nasi.

Kama wanafunzi katika njia ya kuelekea Emau (Luka 24:13-35) panaweza pakawepo nyakati ambazo hatutambui kwamba Mungu yuko pamoja nasi au kwamba uwepo wa Mungu, nguvu zake vinatosha kwa mahitaji yetu.

Lakini Mungu yupo na hata kama mazingira yetu hayabadiliki, uwepo wake, na nguvu zake vinabakia kuwa ni toshelevu.

Maisha yetu na uzoefu wa dunia ni wa tofauti sana na mwandishi wa zaburi. Hata hivyo, tunaweza kuchagua kudai ujasiri unaokuja kutokana na kujua kwamba Mungu ni Mungu, naye ataendelea kuwa Mungu.

Licha ya hofu yetu, tunapokumbuka kazi za Mungu katika historia na katika maisha yetu wenyewe, tunaweza kuwa na uhakika kwamba Mungu ndiye msingi usiotikisika kwa hali yoyote.

*Mpendwa Bwana,*

*Ujasiri wangu uko katika wewe na enzi yako kuu iliyo juu ya vitu vyote. Kati ya changamoto za maisha na kutokuwa na uhakika, nisaidie macho yangu yasibanduke kwako, Mungu asiyetikisika. Katika uwepo wako, napata pumziko nami nadai hili kwangu leo.*

*Asante Yesu.*

*Amina.*

# ‘… NIKIWA PEKE YANGU BARABARANI, NIKIWA NIMEFINYWA NA MZIGO WANGU, YESU MWENYEWE ALINIKARIBIA NA AKATEMBEA NAMI’.

Arch R. Wiggins

Je, huko ‘kutembea na’ kunafananaje kwako?

# kuomba kwa ajili ya mazingira ya migogoro na vita

Hapa kuna mawazo kadhaa ya maombi ambayo unaweza kuyatumia katika muda wako binafsi wa maombi au katika nafasi ya maombi ya kushirikiana.

Tafadhali uwe huru kuyatumia na kuyabadili kulingana na hali yako.

Mawazo yote haya yanalenga kutusaidia sisi kuomba kwa ajili ya mazingira ya migogoro na vita – kwa mazingira na watu walioathirika – na kutusaidia kukumbuka Mungu wetu asiyetikisika ni nani.

## Tulia na Ujue kwamba Mimi ndiye Mungu

Tengeneza mahali pa ukimya na starehe pa kukaa na Mungu katika ukimya.

Unaweza kutengeneza sehemu ya starehe ya kukaa kwenye mito au blanketi, au unaweza kutaka kutumia makaratasi au hema kujenga kibanda huru mbali na usumbufu.

Pata mahali pa kukaa kwa starehe, kulala au kisimama katika sehemu hii ya ukimya na uchukue muda kupumzika katika uwepo wa Mungu.

Tulia.

Tulia na ujue kwamba Mungu ni Mungu.

Unahitaji uache kung'ang'ania nini na badala yake utegemee nguvu za Mungu?



# Vichwa vipya



Kuna watu wengi sana wanaopitia migogoro katika jamii zetu na duniani kote.

Chukua mda upitie magazeti na makala zilizo mbele yako.

Kata kichwa au makala inayokugusa na uibandike kwenye bango. Andika mawazo yako kando yake.

Fanya maombi kwa kichwa cha habari maalum na watu wanaohusika.

Utahitaji:

- mkusanyiko wa magazeti ya hapo, ya kitaifa na kimataifa, au machapisho ya makala za habari.
- mkasi.
- gundi.
- kalamu.
- karatasi za mabango.

Unaposoma, unaweza kupenda kujiuliza mwenyewe maswali haya:

Nini kinatendeka?

Wapi?

Nani anaathirika?

Ni nani viongozi wakuu ambao watakuwa wanajibu?

Mahitaji hivi sasa ni yapi?

# Pumzika katika Kivuli cha Mweza wa Yote.

Zaburi 91:1-2.

Tazama ramani iliyo mbele yako.

Ni wapi katika ramani Mungu anavutia usikivu wako?

Taa ishikilie juu ya ramani.

Tembeza mkono wako mbele ya ramani utengeneze kivuli kwenye ramani juu ya yale maeneo ungependa kuyaombea.

Waombee watu hao wapumzike katika kivuli cha Mweza wa Yote.

Tazama majina ya Mungu na vipengele vya sifa zake zilizopo mbele yako. Unaweza ukahitaji kuongeza ya kwako.

Mungu kwako leo ni nani?

Unavutiwa na majina au sifa zipi?

Kwanini?

Mungu

Aba

Takatifu

Upendo

Yahweh

Bwana

Baba

Muumbaji

Yesu

Mwokozi

Mtetezi

Mweza yote

Alfa na Omega

Mkate wa Uzima

Kristo

Mfariji

Mkombozi

Mtawala

Mkombozi

Mchungaji

Mlinzi

Kimbilio

Yupo siku zote

Jiwe la msingi

Elohim

Mungu wa milele

Mwenye uwezo wote

Mwaminifu

Msingi

Mtoaji

Mwamba

Imanueli

Juu ya yote

Msaidizi

Mimi ni

Yehova

Mfalme wa Wafalme

Mwana kondoo wa Mungu

Simba wa Yuda

Mweza wa yote

Nguvu yangu

Hodari

Nuru

Maisha

Mwongozo

Tumaini

Tabibu Mkuu

Mwanzilishi

Mfalme wa Amani

Baba wa Milele

Ufufuo na Uzima

Haki

Utatu

Mzabibu wa Kweli

Njia, kweli na uzima

Mshauri wa Ajabu

Dunia

Ajabu

Mtetezi

Moto Uteketezao

Siku za Kale

Ukweli

Adonai

Mungu

Huru

Asiyebadilika

Asiyetikisika

Mwenye neema

Mwenye Rehema

Isiyo na Mwisho



# Chini ya Msalaba

Kaa chini ya msalaba.

Umeumizwa, una uchungu, umesalitiwa, umekasirika, umechukia – unaweza kuacha nini hapa?

Acha chochote utakacho hapa. Unataka kukiandika, kukikwaruza na ukiache chini ya msalaba.

Unahitaji kukiri nini? Mwombe Mungu akusamehe.

Unahitaji nini ili usamehe?

Unahitaji kuchukua hatua ipi inayofuata ili kurejesha mahusiano yaliyovunjika?

# Mabadiliko huanza na sisi.

Mabadiliko huanza na sisi.

Andika tendo maalum utakalolifanya kuchangia ipatikane amani (katika mahusiano yangu binafsi, kujielimisha, kuwaelimisha wengine, kujitoa kuomba) na kuliweka kwenye ubao wa kujitoa.

Kujitoa kutatua tofauti na migogoro nyumbani, kazini na labda hata kanisani, kwa amani kupitia kwa mazungumzo na huruma.

Kujitoa kuwatendea wengine kwa heshima, kuonyesha huruma na kuishi kwa masikilizano na wengine.

Kujitoa kuomba mara kwa mara kwa ajili ya dunia na maeneo yenye migogoro.

Najitoa kwa…



‘Nayo nuru yang’aa gizani, wala giza halikuiweza’ – Yohana 1:5

Yesu ndiye Nuru ya Ulimwengu. Mwanga wa Yesu waangaza hata katika mazingira yenye giza nene, ukileta tumaini na mwongozo.

Washa mshumaa kwa ukimya huku ukiombea mgogoro maalum au eneo. Omba wale walio katika mamlaka waone ‘nuru’ na wafanye kazi ili mgogoro ufikie mwisho wake.

SPIRITUAL
LIFE DEVELOPMENT
INTERNATIONAL HEADQUARTERS

Scripture quotations taken from The Holy Bible, New International Version® NIV®
Copyright © 1973, 1978, 1984, 2011 by Biblica, Inc.
Used with permission. All rights reserved worldwide.
Images sourced from pexels.com